
## SEHEMU YA KWANZA : LUGHA

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

**1.** Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 30.
**2.** Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
*(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako* *(iii) Nambari ya KNEC*

***Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1hadi 5***

***(Ni asubuhi wakati wa kipindi cha Kiswahili)***



**Mwalimu:** Hujambo wanafunzi?
**Wanafunzi:** Hatujambo mwalimu. *(Wote wanajibu)*
**Mwalimu:** Juma, hebu tukumbushe aina za maneno ambazo ulisoma wiki iliyopita.
**Juma:** *(Akisimama)* Nomino, vitenzi na vivumishi.
**Mwalimu:** Asante sana. Tumpigie makofi.
**Hamisi:** Je, nomino ni nini?
**Mwalimu:** *(Akielezea)* Nomino ni neno linalotumiwa kutaja mtu, kitu au jambo. Maneno kama vile Juma, Zuia, meza na kitanda ni nomino.
**Hamisi:** Nashukuru mwalimu kwa maelezo yako.

**1.** Kipindi cha Kiswahili kilikuwa wakati gani?
A. Jioni B. Asubuhi
C. Usiku D. Adhuhuri

**2.** Ni mwanafunzi yupi aliyeuliza maana ya nomino?
A. Wanafunzi wote B. Halima
C. Hamisi C. Juma

**3.** Ni nomino ipi ambayo mwalimu hakutaja?
A. Kiatu B. Kitanda
C. Zulia D. Meza

**4.** Juma alitaja aina za maneno zifuatazo isipokuwa
A. nomino B. vitenzi
C. vielezi D. vivumishi

**5.** Ni wanafunzi wawili waliotajwa katika mazungumzo haya. Wataje.
A. Juma na Hamisi B. Juma na Halima
C. Hamisi na Halima D. Mwalimu na Juma

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 6 hadi 10***

Miti ni muhimu sana katika maisha ya wanadamu na wanyama. Mimea humpa mwanadamu chakula na hewa safi anayoipumua. Binadamu hupata chakula kama vile matunda, mboga na nafaka.

Binadamu pia hupata dawa za kiasili ambazo huponya magonjwa mbalimbali. Hakika, dunia bila mimea ni kama binadamu bila uhai.

Isitoshe, miti hutoa kuni kwa matumizi ya kupika. Pia huleta mvua na kuzuia mmomonyoko wa udongo. Tusisahau na mbao ambazo hutumiwa kujengea nyumba na samani kama vile meza, vitanda, sofa na makabati.

Hivyo basi, tupande miti na kutunza iliyopo kwa manufaa yetu sisi.

6. Mimea humpa nini binadamu?
A. Maji ya mvua
B. Hewa safi na chakula
C. Kazi nyingi
D. Vifaa vya ujenzi

7. Kulingana na ufahamu, miti hutupa dawa gani?
A. Za kiasili B. Za miti
C. Za magonjwa D. Za maji

8. Tunafaa kufanya nini kuhusu miti?
A. Kupanda na kutunza
B. Kupanda na kukata
C. Kukata kuni za kupika
D. Kuiuza sokoni

9. Miti kama mimea huzuia nini?
A. Mvua
B. Magonjwa
C. Mmomonyoko wa udongo
D. Chakula

10. Kichwa cha makala haya ni nini?
A. Mifugo na mimea
B. Faida za wanyama
C. Aina ya chakula
D. Umuhimu wa miti

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 11 hadi 15***

Hapo zamani, kobe aliamua kumtembelea rafiki yake fisi. Walikuwa marafiki wa chanda na pete. Mara kwa mara, marafiki hawa walitembeleana ili kujuliana hali.

Siku hiyo, kobe alienda polepole hadi kwa bwana fisi. Bwana fisi alipomwona kobe, alifurahi sana. Mara hii alifurahi kwa sababu alitaka kumla kwani alikuwa na njaa sana. Fisi akamwambia, "Leo lazima uwe kitoweo changu na watoto wangu. Hatuna chakula hapa." Kobe aliposikia hivyo, ghafla akaingiza mwili wake ndani ya kombe lake. Fisi alikasirika asiweze kufanya lolote.

11. Nani waliopendana kama chanda na pete?
A. Fisi na wanawe
B. Kobe na fisi
C. Fisi
D. Kobe

12. Kwa nini wanyama hawa walitembeleana mara kwa mara?
A. Kujuliana hali
B. Kula pamoja
C. Kuongea
D. Kucheza

13. Fisi alipomwona kobe, alifurahi kwa nini?
A. Alimpenda sana
B. Alijua amepata chakula
C. Walikuwa hawajaonana
D. Ili amsalimie

14. Kati ya fisi na kobe, nani alikuwa rafiki mbaya?
A. Kobe
B. Wote
C. Fisi
D. Watoto wao

15. Je, kobe alijificha wapi wakati fisi alitaka kumla?
A. Kwenye shimo
B. Ndani ya nyumba
C. Kwenye kombe lake
D. Alitoroka



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 hadi 20. Chagua jibu lifaalo zaidi kujazia nafasi zilizoachwa wazi***

Wanafunzi ____**16**____gredi ya nne walitembelea kituo ____**17**____redio kilichoko mjini. Walifika kituoni saa tatu ____**18**____ wakiwa na furaha ____**19**____. Siku hiyo, walisoma mambo ____**20**____ kuhusu utangazaji.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | A. wa | B. la | C. cha | D. za |
| **17.** | A. mwa | B. vya | C. za | D. cha |
| **18.** | A. jioni | B. asubuhi | C. adhuhuri | D. alasiri |
| **19.** | A. mwingi | B. wengi | C. nyingi | D. mkubwa |
| **20.** | A. mageni | B. ngeni | C. mgeni | D. wageni |

***Kutoka swali la 21 hadi la 30, jibu kila swali kwa kufuata maagizo uliyopewa***

**21. Andika wingi wa sentensi hii:**
Kitabu changu ni kizuri.
A. Vitabu vyangu ni vizuri.
B. Kitabu vyangu ni vizuri.
C. Vitabu vyetu ni vizuri.
D. Vitabu vyenu ni vizuri.

**22.** Maumbo haya yako katika ngeli gani?
**(Gari, yai, sikio)**
A. KI-VI
B. A-WA
C. LI-YA
D. U-I

**23. Chagua kitenzi katika sentensi hii.**
Mwanafunzi alikimbia kwa kasi.
A. alikimbia
B. mwanafunzi
C. kwa
D. kasi

**24.** Salamu za asubuhi kati ya hizi ni
A. kwa heri
B. shikamoo
C. usiku mwema
D. umeamkaje

**25. Tegua kitendawili kifuatacho:**
Ajua kuchora lakini hajui achoracho.
A. Mchoraji
B. Konokono
C. Kuku
D. Kobe

**26.** Chagua neno ambalo huja kwanza kwenye kamusi.
A. Meza
B. Kitanda
C. Rangi
D. Ua

**27.** Vazi hili huitwaje?



A. Suruali ndefu B. Rinda
C. Kaptura D. Shati

**28.** Ni kifaa kipi hupatikana jikoni?
A. Runinga
B. Zulia
C. Sufuria
D. Kitanda

**29. Kamilisha sentensi hii:**
Mama aliende dukani ________ akanunue mkate.
A. au
B. ili
C. kwa sababu
D. kwa kuwa

**30. Sentensi hii iko katika wakati upi?**
Mama alienda sokoni.
A. Uliopo
B. Ujao
C. Mazoea
D. Uliopita



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**SEHEMU YA B: INSHA**

| JINA LAKE | |
|---|---|

***Andika insha ya kusisimua kuhusu:-***

## SHAMBA LETU



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com